# HRNS yaimarisha msaada kwa wakulima wa kahawa

**Na Mwandishi Wetu,**

MAELFU ya familia za wakulima wadogo wa kahawa nchini Tanzania zinatarajiwa kuendelea kunufaika na programu za muda mrefu za maendeleo ya kilimo na jamii kufuatia mabadiliko ya uongozi katika moja ya taasisi zinazoongoza duniani katika kusaidia kilimo endelevu cha kahawa, Hanns R. Neumann Stiftung (HRNS).

Taasisi hiyo, ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikishirikiana na jamii za wakulima nchini hususani mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kaskazini kuboresha uzalishaji wa kahawa, kuongeza kipato cha kaya, kuhifadhi mazingira na kuibua fursa kwa vijana, imetangaza wiki hii kuwa Dkt. Karen Hadem atajiunga na Jens Sorgenfrei kama Mkurugenzi Mtendaji, akichukua nafasi ya Michael Opitz, anayestaafu baada ya kuiongoza taasisi hiyo kwa zaidi ya miongo miwili kufuatia mpango wa muda mrefu wa kurithishana uongozi.

Kwa jamii za wakulima nchini Tanzania, mabadiliko haya yanakuja wakati HRNS ikiendelea kuimarisha ushirikiano wake na wadau mbalimbali nchini pamoja na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza uzalishaji wa kahawa, kuboresha kipato cha kaya, kuhifadhi mazingira na kuwawezesha vijana.

Akizungumzia mabadiliko hayo, Meneja wa HRNS Tanzania, Morgan Mkonyi, amesema uongozi mpya ni hatua muhimu katika kuhakikisha taasisi hiyo inaendelea kuleta matokeo chanya kwa jamii za wakulima nchini.

"Tunakaribisha kwa furaha mwanzo wa sura hii mpya katika uongozi wa Hanns R. Neumann Stiftung. Chini ya uongozi wa maono wa Michael Opitz, HRNS imekua na kuwa taasisi inayoheshimika duniani, ambayo imebadilisha maisha ya maelfu ya familia za wakulima wadogo, wakiwemo wengi nchini Tanzania. Tunatarajia kushirikiana kwa karibu na Dkt. Karen Hadem pamoja na Jens Sorgenfrei katika kuendeleza msingi huu imara, kuimarisha ushirikiano na kuendelea kuleta matokeo endelevu kwa jamii za wakulima," alisema Mkonyi.

Mabadiliko hayo yanajengwa juu ya msingi uliowekwa na Michael Opitz, ambaye alikuwa na mchango mkubwa katika kuanzishwa na kukuza HRNS hata kabla ya taasisi hiyo kuanzishwa rasmi mwaka 2005. Chini ya uongozi wake, kilichoanza kama miradi ya kuboresha uzalishaji na uchakataji wa kahawa kilikua na kuwa programu pana ya kimataifa inayolenga kuimarisha maendeleo ya jamii za vijijini, ikiwemo Tanzania.

Kwa sasa, HRNS inafanya kazi ya kuwawezesha watu kujenga maisha endelevu kwa kusaidia familia za wakulima wadogo, kulinda bioanuwai na rasilimali za asili, pamoja na kuwapatia vijana fursa za kujenga maisha bora ya baadaye. Taasisi hiyo kwa sasa inatekeleza shughuli zake katika nchi saba za Kusini mwa Dunia (Global South), zikiwemo Tanzania.

Kahawa inaendelea kuwa nguzo kuu ya shughuli za HRNS kutokana na kuwa chanzo kikuu cha kipato kwa mamilioni ya wakulima wadogo duniani. Kadiri miaka ilivyopita, taasisi hiyo imepanua wigo wa shughuli zake kwa kujumuisha uhifadhi wa mazingira, bioanuwai na uwezeshaji wa vijana, ikitambua kuwa maendeleo endelevu ya kilimo yanategemea mazingira salama na jamii zenye uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Akizungumza kuhusu safari yake ya uongozi, Mkurugenzi Mtendaji anayemaliza muda wake, Michael Opitz, alisema mafanikio yaliyopatikana ni matokeo ya ushirikiano wa pamoja.

"Imekuwa heshima kubwa kujenga Hanns R. Neumann Stiftung pamoja na mwanzilishi mwenye maono, timu bora na wadau imara kutoka sehemu mbalimbali duniani. Mafanikio haya yamekuwa juhudi za pamoja zilizowezeshwa na kujitolea kwa wafanyakazi wetu, washirika wetu wa ndani na msaada mkubwa kutoka Bodi ya Wadhamini," alisema.

Jens Sorgenfrei, ambaye amekuwa sehemu ya timu ya uongozi wa HRNS kwa miaka mingi, ataendelea kuhakikisha kunakuwepo mwendelezo wa shughuli za taasisi hiyo, huku Dkt. Karen Hadem akileta uzoefu mkubwa katika ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa na sekta ya uhisani duniani. Kwa pamoja, wanatarajiwa kuiongoza HRNS katika hatua mpya ya ukuaji huku wakiimarisha programu zake za muda mrefu, ikiwemo shughuli zake nchini Tanzania.

Kwa upande wake, Dkt. Karen Hadem alisema anatarajia kuendeleza msingi imara uliowekwa na mtangulizi wake.

"Michael Opitz ameijenga na kuiunda Hanns R. Neumann Stiftung kwa uwazi, uadilifu na matokeo makubwa. Ameacha msingi bora sana. Natarajia kufanya kazi kwa karibu na Jens Sorgenfrei, timu yetu ya kimataifa pamoja na washirika wetu ili kuendeleza kazi ya taasisi na kuongeza kwa njia endelevu mchango wake kwa vijana na familia za wakulima wadogo," alisema.

Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Michael R. Neumann, pia alimpongeza Michael Opitz kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya HRNS.

"Michael Opitz ameijenga Hanns R. Neumann Stiftung tangu mwanzo kwa kujitolea kwa kiwango cha kipekee na amekuwa na mchango mkubwa katika kuunda programu zake. Kwa hilo, ninamshukuru kwa dhati," alisema Neumann.

Aliongeza kuwa uteuzi wa Dkt. Karen Hadem na Jens Sorgenfrei unaunganisha mwendelezo wa mafanikio yaliyopo pamoja na mawazo mapya katika kipindi ambacho ushirikiano wa kimkakati na matokeo yenye tija vinazidi kuwa muhimu katika maendeleo ya kimataifa.

Ikiungwa mkono na mtaji wa kudumu wenye thamani ya takribani euro milioni 150, HRNS imeahidi kuendelea kufadhili kwa muda mrefu programu zinazoboresha maisha ya jamii, kulinda mazingira na kuwapatia vijana fursa mpya katika jamii zinazolima kahawa duniani, ikiwemo Tanzania.



**Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar (kushoto), akisalimiana na Balozi wa Tanzania nchini Nigeria anayesimamia pia shughuli za kibalozi nchini Gambia, Balozi Selestine Kakele, jana wakati alipowasili jijini Banjul nchini Gambia kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa African Caucus wa 2026, utakaofanyika kuanzia leo. (Na Mpigapicha Maalum)**

# DCEA yawanoa wanahabari

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imewanoa waandishi wa habari nchini kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya ikiwemo kemikali bashirifu.

Mafunzo hayo yalifanyika Julai 3,2026 jijini Dar es Salaam, lengo likiwa kuwajengea uwezo wa kuihabarisha jamii kuhusu dawa tiba zenye asili ya kulevya, dawa mpya za kulevya& Maabara Bubu pamoja na Madhara ya Dawa za kulevya.

Akitoa mada kuhusu kemikali bashirifu na dawa za kulevya, Kamishna Msaidizi wa Sayansi Jinai wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Ziliwa Machibya, alizitaja Sheria ya kemikali za Viwandani na Majumbani (Udhibiti na Usimamizi) Na. 3 ya Mwaka 2003.

Nyingine ni Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 (R.E 2020), Vifungu vya (14, 15, 15A) pamoja na Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Na. 1 ya Mwaka 2003 marekebisho ya Sheria ya Fedha 2019).

Alisema, kutokana na sheria hizo alitaja kemikamili bashirifu zilizokamatwa maeneo mbalimbali duniani ni Acetone lita 3360, Ethanol - lita 8750, Azobisisobutyronitrile - kilo 60, Hydrochloric Acid kilo 1400, Lead acetate kilo 5000, N-methylformamide-lita 1890.

Dawa nyingine ni Toluene lita 420, Tartaric acid kilo 375, (2-bromoethyl) benzene kilo 13.5, acetic acidi kilo 4.4, Acetone kilo 22.5, benzyl alcohol kilo 434, ethanol kilo 358, hydrochloric acid 1834.36, methylamine 202.5, tartaric acid kilo 21, toluene kilo 67.5.

Akitoa mifano ya Uchepushwaji nchini, Machibya alisema uchunguzi ulibaini kiasi cha kilo 12 za kemikali bashirifu aina yapseudoephedrine zilikuwa zimechepushwa katika mchakato wa uzalishaji wa dawa za kikohozi na kupelekea uteketezaji wa lita10,000 za dawa zenye pungufu ya kiambata hai cha kemikali hiyo

Pia, alisema ukamatwaji wa tani 21.7 za acetic anhydride nchini Pakistani zilizosafirishwa kutoka Tanzania kwa jina bandia la acetic acid

"Mwaka 2025, jumla ya tani 31.76 na lita 183.500 za kemikali bashirifu zilikamatwa hapa Nchini. Zimezuiliwa kemikali bashirifu tani 734 Kuingia nchini kinyume cha taratibu.

"Kiasi hiki kinahusisha tani 4 za kemikali bashirifu za kutengeneza dawa ya kulevya aina ya fentanaili (kilipangwa kusafirishwa Kwenda Mexico kwa jina bandia la protein biotine).

"Pia, kugundulika kwa maabara bubu ya kutengeneza methafetamine mpakani Namanga upande wa Kenya," alisema Machibya.

# Sekondari tano kufunguliwa Musoma Vijijini

**Na Fresha Kinasa, Mara**

JIMBO la Musoma Vijijini lililopo Mkoa wa Mara linatarajia kukamilisha shule za Sekondari tano mpya na kuanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari 2027, hatua inayotajwa kuwa sehemu ya mkakati wa kupanua upatikanaji wa elimu na kuimarisha ubora wa sekta hiyo jimboni humo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na mbunge wa Jimbo hilo Prof. Sospeter Muhongo kupitia taarifa iliyoitoa. Ambapo shule zitakazofunguliwa ni Kamatondo Sekondari iliyopo Kata ya Nyambono, Rukuba Island Secondary School katika Kata ya Etaro, Mmahare Sekondari iliyopo Kata ya Ifulifu, Mwigombe Technical Secondary School katika Kata ya Kiriba na Kataryo Sekondari iliyopo Kata ya Tegeruka.

Alisema, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya elimu, ambapo imechangia Sh. Mil. 584.28, kwa ajili ya ujenzi wa Kamatondo Sekondari na Sh. Mil. 100, kwa Kataryo Sekondari.

Mbali na mchango wa Serikali, Mfuko wa Jimbo umeendelea kuwezesha ujenzi wa shule hizo kupitia michango ya mifuko ya saruji, mabati na nondo, huku wananchi, viongozi wa maeneo husika pamoja na Mbunge wa Jimbo wakishiriki kwa nguvu kazi na michango mbalimbali ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

Katika Rukuba Island Secondary School, taasisi ya Nyansaho Foundation imechangia mabati 130 ya rangi, huku wananchi wa Kisiwa cha Rukuba wakiendelea kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa shule hiyo. Na upande wa Mwigombe Technical Secondary School, ujenzi unaendelea kwa ushirikiano wa wazaliwa wa Kijiji cha Kiriba, wananchi na Mbunge wa Jimbo, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuongeza shule za ufundi zitakazowapa vijana maarifa na stadi za kujiajiri.

Prof. Muhongo alisema, Kwa sasa, Jimbo la Musoma Vijijini lina shule 33 za sekondari, zikiwemo 31 za Serikali na mbili zinazomilikiwa na madhehebu ya dini. Pia, lina shule nne za kidato cha tano na sita ambazo ni Kasoma, Suguti, Mugango na Mtiro.